Dartmouth-Hitchcock

Kichwa cha Sera	Sera ya Mikopo na Ukusanyaji	Kitambulisho cha Sera	4834
Maneno muhimu	Mikopo, Ukusanyaji, Deni Lisiloweza Kulipwa		

I. Kusudi la Sera

Ili kubainisha jinsi ambavyo Conifer Revenue Cycle Solutions ("Conifer") inapaswa kufuatilia na kukusanya madeni ya akaunti za wagonjwa kama wakala aliyepewa kandarasi wa Dartmouth-Hitchcock Health.

II. Upeo wa Sera

Sera hii inatumika kwa wafanyakazi wote wanaowajibika katika mchakato wa mikopo na ukusanyaji na madeni yote yalitozwa kupitia Dartmouth-Hitchcock Health.

III. Ufafanuzi

Shirika la Ukusanyaji wa Madeni: Mtu mwingine anayekusanya madeni ambayo yanazingatiwa kuwa muda wake wa kulipa umepita.

Mdaiwa: Mtu anayedaiwa.

Kiwango cha Kudai Deni: Kiwango cha mawasiliano na mgonjwa kuhusiana na malipo anayopaswa kulipa. Kiwango cha kudai deni kikiwa cha juu ndivyo deni linapozidi kukaribia kuzingatiwa kuwa muda wake wa malipo umekwisha.

Kutolipa kwa wakati: Deni ambalo halijalipwa kulingana na sheria na masharti ya malipo yaliyobainishwa kwenye taarifa ya malipo, hamna mpango wowote wa kulipa uliowekwa na limeripotiwa katika shirika la ukusanyaji wa madeni.

Mdhamini: Mgonjwa yeyote mwenye umri wa zaidi ya miaka 18 anatambuliwa kama mdhamini, bila kujali mgonjwa ameandikishwa chini ya bima ya nani. Kwa mgonjwa yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18, mzazi au mlezi halali ataorodheshwa kama mdhamani.

ECA: Hatua Isiyo ya Kawaida ya Ukusanyaji wa Deni

Dartmouth-Hitchcock Health: Kwa makusudi ya sera hii, Wanachama wa Mfumo wa Dartmouth-Hitchcock Health (D-HH) ni Alice Peck Day Memorial Hospital, Cheshire Medical Center, Mt. Ascutney Hospital and Health Center, New London Hospital na Visiting Nurse na Hospice for Vermont and New Hampshire (VNH). Hospitali zingine zote zinazopatikana New Hampshire na Vermont zinachukuliwa kuwa Si vituo Wanachama.

Kuanzia tarehe 11 Mei 2019, sera hii inatumika katika Dartmouth-Hitchcock Clinic, Mary Hitchcock Memorial Hospital, Alice Peck Day Memorial Hospital, New London Hospital na Cheshire Medical Center.

Kuanzia tarehe 10 Oktoba 2020, sera hii pia inatumika katika New London Hospital.

IV. Taarifa ya Sera

- D-HH hujaribu mara kwa mara kukusanya maelezo ya hivi karibu zaidi ya bima ya Mdhamini wa mgonjwa na kuthibitisha huduma zinazoshughulikiwa na bima na malipo ambayo mgonjwa anapaswa kulipa mwenyewe kupitia zana zilizopo za uthibitishaji wa bima na manufaa.
- Malipo yanayopaswa kulipwa na mgonjwa mwenyewe kama vile malipo ya bima yanayoshirikiwa malipo ya lazima hukadiriwa na mipango ya malipo kuwekwa kabla ya kutolewa kwa huduma au wakati wa kutolewa kwa huduma.
    - Mgonjwa anaweza kuwa na chaguo la kulipa gharama anazopaswa kulipa mwenyewe baada ya kupokea huduma.
    - Huduma zingine zinaweza kuhitaji mgonjwa alipe mapema (k.m., Urembo, vifaa vya kusaidia kusikia, n.k.).
- Kwa madeni yoyote ambayo hayajalipwa, D-HH itatoa taarifa ya malipo na kuomba malipo yalipwe kikamilifu.
- Malipo ya polepole yanakubaliwa muradi masharti ya kiwango cha chini zaidi cha malipo yafuatwe kama ilivyobainishwa katika utaratibu wa mpango wa bajeti. Soma “Utaratibu wa Mpango wa Malipo ya Bajeti na Kurejeshwa: Kitengo cha Kusimamia Ushuru” (kiungo kilicho hapa chini)
- Madeni yanayopaswa kulipwa yanaweza kuripotiwa katika shirika la ukusanyaji wa madeni wakati ambapo madeni hayo yanazingatiwa kuwa hayawezi kulipwa na wakati huo, madeni yanayoripotiwa katika shirika la ukusanyaji wa madeni huzingatiwa kuwa muda wake wa kulipa umekwisha au madeni ambayo yanapaswa kulipwa yanaweza kuainishwa kama madeni yasiyoweza kulipwa.

A. Madeni ya Kulipa Mwenyewe

- Madeni ya kulipa mwenyewe yanawakilisha gharama ambazo zinapaswa kulipwa na Mdhamini.
- Haya ni pamoja na, wala si tu:
    - Madeni yaliyo kwenye akaunti za watu wasio na bima
    - Madeni yaliyosalia baada ya malipo ya bima au ya watu wengine ikijumuisha:
        - Gharama zinazozingatiwa kama huduma zisizoshughulikiwa na bima kama ilivyobainishwa na mpango wa bima ya mgonjwa
        - Malipo yanayoshirikiwa
        - Malipo ya bima yanayoshirikiwa
        - Malipo ya lazima
    - Wadhamini wanaotoza bima yao wenyewe na kuamua kutoipa D-HH ruhusa ya kutoza bima yao
    - Huduma za ziada za mgonjwa

B. Kuhamishiwa kwenye Malipo ya Kulipa Mwenyewe

- Madeni huhamishiwa kwa Mdhamini na taarifa hutumwa tu baada ya malipo ya huduma kulipwa na walipaji wengine, isipokuwa masharti yafuatayo yatimizwe:
    - D-HH imeshindwa kushawishi mlipaji kulipa deni, licha ya kujaribu mara kwa mara kuomba malipo.
    - D-HH imearifiwa na mtoa huduma huyo mwingine wa bima kuwa Mdhamini hajajibu maombi ya kutoa maelezo yanayohitajika ili deni kulipwa.
    - Mdhamini anatoa maelezo ya bima yasiyo sahihi. Taarifa ya kwanza itakayotolewa kwa mgonjwa itatoa nambari ya simu ya huduma kwa wateja na ombi la kusasisha maelezo ya bima

ikiwa si sahihi.

C. Taarifa za Malipo ya Mgonjwa

- Kwa sasa Wadhamini wanapokea taarifa kama ifuatavyo:
  - Resolute Hospital Billing
    - Huduma zote za hospitali na ziara zote za kutembelea Ofisi ya MD hospitalini.
  - Resolute Professional Billing
    - Ada za kitaalamu kwa watoa huduma (bila kujumuisha huduma za wagonjwa wasiolazwa za hospitali, ikijumuisha huduma za matibabu ya meno).
- Ufuatao ni mwongozo wa jumla wa utoaji wa taarifa za huduma za hospitali na kliniki:
  1. Taarifa hutolewa kila mwezi.
  2. Taarifa zote hutolewa katika kiwango cha Mdhamini, hali inayomaanisha kuwa ziara nyingi au ankara nyingi zitaorodheshwa kwenye taarifa moja.
  3. Tarehe za kutolewa kwa taarifa inayofuata na viwango vya kudai deni huwekwa kabla ya kutolewa kwa taarifa kulingana na malipo yaliyochapishwa.
  4. Ili kusitisha mawasiliano ya kudai deni, lazima kiwango cha chini zaidi cha malipo kilipwe ambacho kinaweza kuhusiana na mpango wa bajeti uliobainishwa.
  5. Wadhamini wanaotimiza masharti ya kiwango cha chini zaidi cha malipo kwa wakati hawatapokea taarifa ya kudai deni kwenye kiwango kinachofuata.

D. Kuripotiwa katika Shirika la Ukusanyaji wa Madeni

- D-HH haitatumia hatua zisizo za kawaida za ukusanyaji wa madeni (ECA) kama vile kuripoti kwa mashirika ya kuripoti mikopo kabla ya kufanya juhudi za kubainisha iwapo mgonjwa anatimiza masharti ya kupokea msaada wa fedha. Mgonjwa ataripotiwa kwenye shirika la ukusanyaji wa madeni baada ya kubainisha iwapo mgonjwa huyo anatimiza masharti ya kupokea msaada wa kifedha (hii ni pamoja na matumizi ya ustahiki unaokisiwa). Hali zozote maalum zinapaswa kuidhinishwa na Afisa Mkuu wa Fedha. Ili upate maelezo kuhusu hali ya kutimiza masharti ya kupokea msaada wa kifedha, tafadhali soma “Sera ya Msaada wa Fedha kwa Huduma za Afya” (angalia kiungo kilicho hapa chini). Nakala zinapatikana mtandaoni au unaweza kuomba katika Ofisi za Huduma za Fedha kwa Wagonjwa au unaweza kutumiwa kwa njia ya barua kwa kupiga simu kwa 844-808-0730.
- D-HH haitachukua hatua ya kuripoti madeni kwenye shirika la ukusanyaji wa madeni hadi zikiwa zimepita angalau siku 120 baada ya kutumwa kwa taarifa ya kwanza ya malipo baada ya mgonjwa kuruhusiwa kuondoka hospitalini na D-HH itatuma notisi zikiwa zimesalia angalau siku 30 kabla ya kutuma taarifa ya ukusanyaji wa deni.

E. Ufadhili kwa misingi ya Kukisia

D-HH inaweza kutumia watu wengine kukagua maelezo ya mgonjwa ili kutathmini mahitaji yake ya fedha. Ukaguzi huu hutumia muundo wa ubashiriki unaotambulika na sekta ya huduma ya afya ambao unatokana na hifadhidata za rekodi za umma. Muundo huu hutumia rekodi ya data ya umma ili kutathmini kiwango cha uwezo wa kifedha na uchumi wa jamii ambayo inajumuisha makadirio ya mapato, rasilimali na uwezo wa kupata pesa. Kikundi cha kanuni za muundo kimebuniwa ili kutathmini kila mgonjwa kwa kutumia viwango sawa na hupimwa kulingana na kumbukumbu za mara za kuidhinishwa kwa maombi ya msaada wa fedha ya mfumo wa Dartmouth-Hitchcock Health.

Maelezo kutoka kwenye muundo wa ubashiri yanaweza kutumiwa na D-HH kutoa ustahiki kwa misingi ya kukisia katika hali ambapo hakuna maelezo yaliyotolewa moja kwa moja na mgonjwa. Msaada wa fedha kwa misingi ya kukisia haupatikani kwa ajili ya kulipa madeni ambayo hayakushughulikiwa na bima ya Medicare.

Uchunguzi kwa msingi wa kukisia hutumiwa, bila kujali deni lililopo, kwenye akaunti zinazotimiza masharti zilizokaa kwa zaidi ya siku 120 baada ya kutolewa kwa taarifa, baada ya kutolewa kwa notisi za kukusanya deni na kabla ya akaunti kuelekezwa kwa shirika la nje la ukusanyaji wa madeni ili kutoa msaada wa fedha kwa wagonjwa ambao hawajakuwa wakijibu mawasiliano ya taarifa za chaguo la kujaza Fomu ya Maombi ya Msaada wa Fedha.
Akaunti za kurithisha mali za walioaga dunia ambazo zimepitisha vikomo vya muda zinatimiza masharti ya uchunguzi kwa misingi ya kukisia.

Ufadhili kwa misingi ya kukisia hauchukui nafasi ya michakato ya kawaida ya FAP; hutumiwa kutoa mchango wa ziada katika juhudi hizi na unalenga wagonjwa ambao vinginevyo hawajibu mawasiliano ya mchakato wa kawaida wa FAP. Katika juhudi za kuondoa vizuizi kwa wagonjwa hawa na kuboresha manufaa tunayowapa wagonjwa, hospitali hutumia mchakato wa uchunguzi wa mtandaoni kabla ya kuwekwa kwenye orodha ya akaunti za madeni yasiyoweza kulipwa. Wagonjwa wanaotimiza masharti ya ufadhili kwa misingi ya kukisia hawataripotiwa kwa shirika la ukusanyaji wa madeni.

Mchakato wa kujumuishwa katika mpango unalingana na algoriti za kutoa alama kwa kutumia maelezo ya rekodi ya umma na kwa kawaida hautumii kipimo cha ada zinazobadilika. Mapunguzo yasiyo kamili hayaruhusiwi na Ufadhili kwa Misingi ya Kukisia. Watu mahususi wanaokusudiwa ni pamoja na:

- Walioaga dunia wasio na mali au familia inayojulikana
- Watu wasio na makao ya kudumu
- Watu waliotenganishwa na familia wasiopokea msaada wowote
- Wagonjwa ambao hawajibu mawasiliano au wasioweza kukamilisha mchakato wa kawaida

Mchakato wa kutoa alama za kupokea ufadhili kwa msinigi wa kukisia hutumia kigezo cha uchumi wa jamii na data isiyotokana na mikopo. Mchakato wa uchunguzi hutumia hifadhidata ya umma yenye maelezo yafuatayo:

- Shughuli za Mtumiaji
- Rekodi za Mahakama
- Umiliki wa Mali
- Umiliki wa nyumba dhidi ya mkodishaji
- Data ya takwimu za watu, uchumi wa eneo
- Hali ya ajira
- Faili za Huduma za Umma
- Faili za
- Serikali (Hali ya kufilisika, SSN, watu walioaga dunia)

Ufadhili kwa msingi wa kukisia hautegemei data ya ripoti ya ofisi ya mikopo na huondoa maombi ya kuangalia alama ya mikopo kwenye ripoti ya mkopo. Maelezo yaliyopatikana hujumuisha alama ya Ufadhili kwa Msingi wa kukisia ya 0 (anayeihitaji zaidi) hadi 1000 (asiyehitaji sana). Maelezo hayo

hubashiri mahitaji ya kuwa na mdhamini kulingana na vigezo vinavyojulikana ikiwa ni pamoja na, wala si tu Mapato, Mali na Uwezo wa kupata pesa.

Ubainishaji wa akaunti zinazotimiza masharti

- Alama ya malipo itawekwa kwenye akaunti zinazotimiza masharti
- Akaunti zinazotimiza masharti ya bima ya Medicare hazitajumuishwa
- Ikiidhinishwa, misimbo ya marekebisho ya EPIC itatumiwa kutambua akaunti zinazotimiza masharti
    - 5027 Matibabu ya Bila Malipo kwa msingi wa kukisia baada ya bima na msimbo
    - 5026 Matibabu Bila Malipo kwa Msingi wa Kukisia

F. Sera ya Mikopo ya Mtoa Huduma

- D-HH ina aina tatu zifuatazo za akaunti za wateja/watoa huduma:
    - Akaunti za utafiti
    - Akaunti za wateja za kibiashara (yaani, Hospice, SNF, City Accounts, Lab, nk.).
    - Akaunti za Afya ya Kikazi ambazo zina mkataba wa huduma unaohitajika na mwajiri kama masharti ya kuajiriwa zitalipiwa na mwajiri.
- Taarifa za kila mwezi hutolewa na zinapaswa kulipwa kikamilifu ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya kutolewa kwa taarifa.
- Hamna mipango ya bajeti itakayowekwa kwenye akaunti hizi.
- Akaunti ambazo zimekaa kwa zaidi ya siku 30 hutumiwa barua inayoonyesha pesa zinazopaswa kulipwa ambazo muda wake umepita na hutumiwa notisi inayosema kwamba hatua ya kuendelea kuchelewa kulipa inaweza kusababisha kuwekwa kwa gharama za riba katika kiwango cha 1.5% kwa mwezi kwenye madeni yote ambayo yanastahili kulipwa.
- D-HH ina haki ya kuripoti akaunti zenye madeni kwenye Mashirika ya Ukusanyaji wa Madeni.

G. Akaunti za Kufilisika

- Aina mbili za notisi za kufilisika hutumwa na Mahakama ya Kesi za Kufilisika:
    - Notisi ya kuanza kuwasilisha kesi
    - Kuondolewa/Kufutiliwa mbali kwa deni la mdaiwa
- Baada ya D-HH kuarifiwa kuhusu kuwasilishwa kwa kesi ya kufilisika, lazima juhudi zote za ukusanyaji wa deni zikomeshwe.
- Notisi ya kuanza kusikilizwa kwa kesi hupokewa na D-HH.
    - Uwasilishaji wa kesi unaweza kufanywa na mtu binafsi au na watu wawili na watoto hawapaswi kutajwa.
    - Wanafamilia wote lazima watambuliwe na kila akaunti lazima iarifiwe kwamba vikao vya kusikilizwa kwa kesi ya kufilisika vimeanza na tarehe ya kuwasilishwa kwa kesi hiyo.
    - Ikiwa akaunti yoyote imeripotiwa kwenye shirika la nje la ukusanyaji wa madeni, lazima shirika na akaunti hiyo viarifiwe na nakala ya kesi hiyo itumwe katika mahakama ya kesi za kufilisika ili iwekwe kwenye rekodi.
    - Gharama zote zilizobainishwa kwenye notisi zitajumuishwa kwa madhumuni ya uamuzi wa kesi ya kufilisika.
    - Gharama zote zinapaswa kusasishwa kulingana na kiwango cha fedha za kufilisika.

- Kesi ya kufilisika ikiamuliwa, mahakama itatuma notisi ya kufutiliwa mbali au kutofutiliwa mbali kwa deni.

  Katika hali ambapo deni halitafutiliwa mbali, D-HH inaweza kuendelea na shughuli ya ukusanyaji wa deni.
  - D-HH ikipokea notisi ya kufutiliwa mbali kwa deni, lazima turekebishe deni lolote lililo kwenye mfumo wa Epic.
  - Akaunti zote zinazohusishwa na kesi husika ya kufilisika lazima ziarifiwe kuhusu uamuzi wa mwisho uliotolewa.
  - Mashirika ya ukusanyaji wa madeni yataarifiwa na kutumiwa hati zozote za kuthibitisha.

H. Madai ya Kesi

- D-HH itakomesha ufuatiliaji wa madeni yanayopaswa kulipwa na mgonjwa au kudai malipo ya kutii ya akaunti zilizowasilisha kesi mahakamani baada ya kupokea Barua ya Ulinzi (LOP) iliyotumwa na wakili anayewakilisha mgonjwa inayosema kwamba aliyewasilisha kesi mahakamani atalinda maslahi ya D-HH katika malipo yoyote baadaye.
- Ikiwa deni halitafutiliwa mbali, deni litarejeshwa kwa mdhamini na mipango ya kulipa kuwekwa.
- D-HH ina haki ya kuwasilisha kesi ya dai la kumiliki mali katika kesi za madeni kwa maslahi ya hospitali.

V. Marejeleo - HAMNA

Mmiliki Anayewajibika:	Kitengo cha Kusimamia Ushuru	**Mtu wa kuwasiliana naye:**	Kimberly Mender
Imeidhinishwa Na:	Bodi ya Wadhamini; Afisa Mkuu - Fedha; Ofisi Inayoshughulikia Sera (OPS); Kays, Kieran; Naimie, Tina	**Toleo la #**	8
Tarehe ya Sasa ya Kuidhinishwa:	11/03/2020	**Kitambulisho cha Hati ya Zamani:**	RMD.0025
Tarehe ya Sera Kuanza Kutumika:	11/03/2020		
Sera na Taratibu Husika:	Taratibu za Mpango wa Malipo ya Bajeti na Kurejeshwa: Kitengo cha Kusimamia Ushuru Sera ya Msaada wa Fedha za Huduma za Afya		
Zana za Usaidizi wa Kazi Husika:			